

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA
MICHEZO KWA KUSHIRIKIANA NA WIZARA YA
AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIWA NA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU UGONJWA WA CORONA (COVID-19)



Aprili 2020

YALIYOMO

DIBAJI: -----	II
SHUKRANI:-----	III
UTANGULIZI:-----	1
UGONJWA WA CORONA (COVID – 19), DALILI ZAKE NA NAMNA YA KUJIKINGA.----	2
UMUHIMU WA KUSHIRIKISHA VYOMBO VYA HABARI KUKABILIANA NA JANGA LA CORONA -----	4
MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIWA WAKATI WA KURIPOTI TAARIFA ZA UGONJWA WA CORONA (COVID- 19)-----	5
MAMBO YANAYOKUBALIKA -----	5
MAMBO YASİYOKUBALIKA -----	6
WAMILIKI WA VYOMBO VYA HABARI NA USALAMA WA WATUMISHI -----	7
WAJIBU WA WAANDISHI WA HABARI NA WAPIGA PICHA KUJILINDA NA UGONJWA WA CORONA -----	9
MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KWA WANAOKWENDA KURIPOTI HABARI ZA UGONJWA WA CORONA KWENYE MAENEO HATARISHI -----	11
MAMBO YA KUZINGATIA KATIKA KUHAKIKISHA MAKUNDI MAALUM YA JAMII (WALEMAVU, WAZEE, WANAWAKE, WATOTO NA JAMII ZA PEMBEZONI) WANAPATA ELIMU YA UGONJWA WA CORONA:-----	13
Watoto: -----	13
Watu wenye ulemavu: -----	14
Wanawake na wasichana:-----	14
Wazee: -----	14
Watu wenye magonjwa sugu:-----	15
Jamii za pembezoni:-----	15
Unyanyapaa, ubaguzi na uzushi katika jamii:-----	16
HITIMISHO:-----	17

DIBAJI

Maelezo haya muhimu ya kuzingatiwa kuhusu ugonjwa wa Corona yameandikwa maalumu kwa waandishi wa habari na vyombo vya habari. Serikali imeamua kuandaa maelezo haya kwa ajili ya vyombo vya habari kutokana na umuhimu na majukumu yake ya kuelimisha na kuhabarisha jamii namna ya kujingika kupata ugonjwa wa Corona na hatua za kuchukua mara wanapoon dalili za ugonjwa huo. Vyombo vya habari vinatumika kutoa taarifa mbalimbali zinazohusu mwenendo wa ugonjwa na maelekezo muhimu yanayotolewa na Serikali na wataalam wa afya kwa lengo la kukabiliana na ugonjwa huo tishio kwa taifa na dunia nzima.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefanya juhudi kubwa kudhibiti kusambaa kwa ugonjwa huu ndani ya mipaka ya Tanzania kwa kuhamasisha wananchi kuchukua hatua za kujilinda kwa kuzingatia usafi wa mikono, kupunguza mikusanyiko ya watu, kufunga shule zote kuanzia Elimu ya msingi hadi Chuo kikuu, kuimarisha uwezo wa kupima maambukizi ya virusi vya homa ya Corona kwa njia za kisasa na kuimarisha uwezo wa ufuatiliaji wa wahisiwa na wagonjwa wa Corona. Pia Serikali imetenga maeneo maalumu nchi nzima kwa ajili ya wahisiwa na wagonjwa wa ugonjwa wa Corona.

Maelezo haya yanaainisha mambo muhimu ya kutekelezwa na vyombo vya habari katika kipindi cha kukabiliana na ugonjwa wa Corona na yanasaidia kumpa kila mwandishi wa habari elimu na ujuzi wa kujikinga na kuikinga jamii dhidi ya ugonjwa wa Corona. Maelezo haya muhimu pia yanafafanua kwa uwazi maeneo ambayo mwandishi wa habari anapaswa kutoa ushirikiano katika kuelimisha jamii na namna ambavyo vyombo vya habari na watumishi wake watajikinga na maambukizi ya ugonjwa huo wakiwa kazini.



Dkt. Hassan Abbasi
Katibu Mkuu

Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo

SHUKRANI

Maelezo haya kwa vyombo vya habari kuhusu ugonjwa wa Corona ni zao la juhudi za pamoja zilizojumisha wataalamu mbalimbali, kutoka maeneo mbalimbali waliofanya kazi kwa weledi ili kuhakikisha tasnia nzima ya habari inapata maelezo ya kina ya namna ya kutekeleza majukumu yao katika kipindi hiki cha mlipuko wa ugonjwa wa Corona.

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo inapenda kutoa shukrani za dhiti na kutambua mchango wa kila mmoja aliyeshiriki katika kuandaa na kukamilisha maelezo haya.

Serikali kupitia Wizara zinazosimamia Tasnia ya Habari na sekta ya Afya inapenda kutambua mchango wa kipekee kwa timu maalum iliyoshiriki kuandaa maelezo haya na mchango wa UNESCO katika kuchapisha maelezo haya muhimu kwa sekta ya afya na tasnia ya habari.

Shukrani za pekee zinatolewa kwa kamati ndogo ya mawasiliano wakati wa majanga na ushirikishwaji jamii pamoja na kamati ya Wizara ya Afya ya kudhibiti magonjwa ya dharura kwa kufanikisha upatikanaji wa maelezo haya. Ni matumaini yangu maelezo haya yatatoa elimu na ujuzi sahihi kuhusu ugonjwa wa Corona kwa kila mwandishi wa habari, wamiliki na viongozi wa vyombo vya habari nchini ambavyo vimekuwa mstari wa mbele kutoa elimu kwa umma kuhusu janga la ugonjwa wa Corona.



Dkt. Hassan Abbasi
Katibu Mkuu

Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo

SURA YA 1

Utangulizi

Dunia, Tanzania ikiwemo ipo katika kipindi kigumu cha mlipuko wa ugonjwa unaosababishwa na aina mpya ya virusi vya Corona ulioanza mwaka 2019 na kupewa jina la ugonjwa wa Corona (Corona Virus Disease 2019 au COVID-19).

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kama zilivyo nchi nyingine duniani zikiwemo za Afrika Mashariki, ipo katika mapambano dhidi ya ugonjwa huu ambao umeingia nchini tangu tarehe 16 Machi, 2020. Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, imeona umuhimu wa waandishi wa habari na wadau wengine kushirikiana katika kupambana na ugonjwa wa Corona. Waandishi wa habari wana jukumu la kutoa taarifa sahihi kwa jamii wakati wote na umakini zaidi unahitajika katika uandishi wa habari za majanga.

Serikali imeamua kuandaa maelezo haya muhimu kwa ajili ya vyombo vya habari kutokana na umuhimu wake na majukumu ya kuelimisha na kuhabarisha jamii namna ya kujikinga dhidi ya ugonjwa wa Corona na hatua za kuchukua mara wanapooa dalili za ugonjwa huo. Vyombo vya habari vinatumika kutoa taarifa mbalimbali zinazohusu mwenendo wa ugonjwa na maelekezo muhimu yanayotolewa na Serikali na wataalam wa afya kwa lengo la kukabiliana na ugonjwa huu ambao ni tishio kwa Taifa na dunia nzima.

Maelezo haya yaliyopo katika andiko hili yanaainisha mambo muhimu ya kutekeleza na waandishi wa habari katika kipindi cha kukabiliana na ugonjwa wa Corona ambapo kuna changamoto nyingi miongoni mwa jamii ambayo ina uelewa mdogo kuhusu ugonjwa huu. Baadhi ya changamoto hizo ni; wananchi kukifikiria kila kikohozi na mafua ni ugonjwa wa Corona, kutozingatia maelekezo ya kujiepusha na misongamano, unyanyapaa kwa watu waliopona na baadhi ya watu kutoafiki taratibu na miongozo ya karantini. Aidha, kuna dhana potofu miongoni mwa jamii dhidi ya ugonjwa huu kama vile; waafrika hawawezi kuathirika na ugonjwa wa Corona, kujamiiana kunazuia ugonjwa wa Corona na unywaji wa pombe unazuia kupata ugonjwa wa Corona.

Kutokana na changamoto hizi, Serikali imeandaa maelezo haya mafupi kueleza maeneo ambayo mwandishi wa habari anapaswa kutoa ushirikiano katika kuelimisha jamii na namna ambavyo vyombo vya habari na watumishi wake watatekeleza ili kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huu.

Maelezo haya muhimu yatahusu wamiliki, viongozi na waandishi wa habari wa magazeti, redio, runinga na mitandao ya kijamii inayosambaza taarifa za ugonjwa wa Corona kwenda kwa jamii.

SURA YA 2

UGONJWA WA CORONA (COVID – 19), DALILI ZAKE NA NAMNA YA KUJIKINGA.

Ugonjwa wa Corona (COVID-19) ni ugonjwa unaosababishwa na aina mpya ya virusi vya Corona. Mlipuko wa ugonjwa huu ulianza mwishoni mwa mwezi Desemba 2019 katika mji wa Wuhan uliopo China na kusambaa duniani kote.

Dalili za ugonjwa wa Corona ni; homa, kikohozi kikavu, mafua, mwili kuchoka, kupumua kwa shida, kubanwa mbavu na maumivu ya viungo. Ugonjwa huu hauna tiba maalum, bali mgonjwa hupatiwa matibabu kulingana na dalili zake.

Ili kujikinga na kuzuia kusambaa kwa maambukizi ni muhimu kila mmoja wetu kuzingatia kanuni za Afya ambazo ni;

- ♦ Funika mdomo na pua wakati wa kukohoa kwa kutumia sehemu ya ndani ya kiwiko cha mkono na kuepuka kugusa macho, pua na mdomo;




- ♦ Nawa mikono mara kwa mara kwa maji yanayotiririka na sabuni au kwa kutumia vitakasa mikono (Sanitizer).



- ♦ Epuka kusalimiana kwa mikono; kubusiana na kukumbatiana;



- Kaa umbali zaidi ya mita moja (1) kati ya mtu na mtu;



- Epuka mikusanyiko; na
- Epuka safari zisizo za lazima kwenda maeneo yaliyoathirika ndani na nje ya nchi na inapolazimu kusafiri jitahidi upate maelezo ya kitaalamu kabla ya kuanza safari.



SURA YA 3



UMUHIMU WA KUSHIRIKISHA VYOMBO VYA HABARI KUKABILIANA NA JANGA LA CORONA

Vyombo vya habari vikiwemo; redio, runinga, magazeti na mitandao ya kijamii ni muhimu katika kutoa habari za kuelimisha jamii kuhusu ugonjwa wa Corona. Vyombo hivi vinapaswa kutekeleza majukumu yake kwa weledi, usahihi na bila kupotosha umma kwa kuripoti taarifa zilizotolewa na wenye mamlaka ya kutoa taarifa hizo.

Vyombo vya habari nchini vikitekeleza wajibu wake vinaweza kuleta mabadiliko na mafanikio ikiwa ni pamoja na; kuokoa maisha ya watu, kuimarisha juhudi za kuwasaidia wanajamii katika kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huo, kuwapa wagonjwa na waliopona matumaini, kuimarisha uhusiano kati ya jamii na watoa huduma, kukabiliana na dhana potofu, kuhakikisha matarajio ya jamii yanafikiwa na kuwapa wanajamii wa kawaida fursa ya kutoa maoni wakati wa mlipuko wa ugonjwa huu.



SURA YA 4

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIWA WAKATI WAKURIPOTI TAARIFA ZA UGONJWA WA CORONA (COVID- 19)



Serikali imetoa maelezo haya muhimu kwa vyombo vya habari katika kuripoti masuala yanayohusu ugonjwa wa Corona nchini ambayo yanapaswa kuzingatiwa pamoja na Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari(2016), Sheria ya Makosa ya Mtandao(2015), Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa(2016) na miongozo mingine inayotolewa na taasisi zenye mamlaka ikiwa ni pamoja na Shirika la Afya Duniani (WHO), Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mingine ya nchi. Vyombo vya habari pia vina wajibu wa kusimamia maadili na weledi katika kuripoti taarifa za janga la Corona. Vyombo hivyo vyenye nguvu na ushawishi mkubwa visipotekeleza majukumu yake kwa weledi na maadili, vinaweza kusababisha taharuki na janga kubwa

miongoni mwa jamii. Ili kufanikisha azma ya kutoa elimu ya kukabiliana na ugonjwa wa Corona, yafuatayo yanapaswa kutekelezwa na vyombo vya habari nchini;

4.1 MAMBO YANAYOKUBALIKA

- i) Kupata taarifa sahihi zenye ukweli kwa kutumia vyanzo sahihi vya habari vya kuaminika ambavyo ni; Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Waziri wa Afya na Msemaji Mkuu wa Serikali. Wataalam wa Afya wanaweza kutumiwa kutoa ufafanuzi wa kitaalam kuhusu ugonjwa wa Corona.
- ii) Kuzingatia maadili, taratibu na miiko ya kitaaluma.
- iii) Kuelewa mipango na mikakati ambayo inatekelezwa katika juhudi za kupambana na janga la ugonjwa wa Corona na athari zake kijamii na kiuchumi.
- iv) Kuheshimu waathirika wa ugonjwa wa Corona na kujali haki yao ya faragha kwa kupunguza mahojiano nao, kutowapiga picha na kutaja majina yao katika habari zinazowahusu bila ridhaa yao wanapotaka kueleza uzoefu wao ili jamii ijue bayana juu ya kadhia iliyowasibu.
- v) Kuhakikisha picha au vielelezo vinavyotumika katika taarifa za habari kuhusu ugonjwa wa Corona ni sahihi na vinaakisi hali halisi iliyopo.
- vi) Kuripoti na si kufanya uchambuzi utakaopotosha kwa sababu ya kukosa uelewa wa kutosha kuhusu ugonjwa huo labda tu pale uchambuzi unapokuwa umetokana na maoni ya wataalamu wa sekta ya afya wenye uelewa wa kutosha kuhusu ugonjwa huo.
- vii) Kuwa makini katika uandishi wa vichwa vya habari ili visipotoshe taarifa;
- viii) Kutumia takwimu na vielelezo kwa umakini na usahihi kulingana na muktadha husika ili kuepusha hofu miongoni mwa jamii.
- ix) Kuthibitisha ukweli wa taarifa ili kuepuka kusambaza taarifa potofu.

x) Kuwa makini na kuchukua tahadhari kwenye matukio kwa kuzingatia amri ya Serikali inayokataza mikusanyiko na mambo mengine yasiyoruhusiwa.

xi) Kuwa mwangalifu na aina ya usafiri unaotumia wakati wa kwenda kukusanya habari na kurejea ofisini ili kuepuka msongamano unaowaweka watu kwenye hatari ya kupata maambukizi.

4.2 MAMBO YASİYOKUBALIKA

i) Kuandika taarifa zisizo sahihi zilizopatikana kwenye vyanzo visivyo na uhakika.

ii) Kuandika na kusambaza taarifa na takwimu za uongo zenye kuleta taharuki.

iii) Kutumia lugha au viashiria vya ubaguzi wa rangi, dini, kabila au taifa katika taarifa au kutoa habari kwa namna ambayo inaweza kusababisha athari kwa mtu, kabila, dini au taifa lililobaguliwa.

iv) Kushiriki bila kufuata taratibu na miongozo muhimu kwenye kazi zinazofanyika kwenye maeneo hatarishi yanayoweza kusababisha kupata maambukizi ya ugonjwa wa Corona.

v) Kutovaa mavazi ya kujikinga na maambukizi wakati wa kuripoti ndani ya eneo lenye wagonjwa wa Corona (Isolation Area) au maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya wahisiwa wa ugonjwa wa Corona (Karantini).

vi) Kukaa karibu na mtu yeyote mwenye kuonyesha dalili za kuwa na maambukizi ya njia ya hewa, kama vile kikohozi na kupiga chafya na kushiriki kazi kwenye mikusanyiko bila kuvaa vifaa kinga.

vii) Kukaribiana chini ya mita moja (1) na mtu anayehojiwa katika kipindi hiki cha mlipuko wa ugonjwa wa Corona.


**Jikinge, Wakinge Wengine
CORONA INAZUILIKA**

Zaidi kuhusu Corona piga **199**

au piga ***199#**



SURA YA 5



WAMILIKI WA VYOMBO VYA HABARI NA USALAMA WA WATUMISHI

Kwa mujibu wa Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka (2016) vyombo vya habari vina wajibu wa kutoa huduma za habari kwa jamii. Waandishi wa habari wamekuwa mstari wa mbele katika kuhabarisha umma kuhusu ugonjwa wa Corona.

Kutokana na kujitokeza kwa mazingira hatarishi kwa watumishi, baadhi ya makampuni yameamua kuruhusu wafanyakazi wao kufanyakazi kwa njia ya mtandao. Hata hivyo, kutokana na hali halisi ya utendaji kazi wa vyombo vya habari unaomlazimu mwandishi wa habari kufuata taarifa kwa mhusika na wakati mwingine eneo hatarishi ili kupata picha na sauti ya watoa habari, vyombo vya habari nchini bado vinawahitaji watumishi wake kwenda kazini kufanya kazi. Pamoja na kuheshimu juhudi na majukumu ya vyombo vya habari nchini katika kutekeleza majukumu yake, Serikali inathamini afya ya wananchi wake wakiwemo waandishi wa habari hivyo inawashauri wamiliki wa vyombo hivyo nchini kuona umuhimu wa kuwalinda watumishi wake kutokana na hatari ya maambukizi ya ugonjwa wa Corona.

Ili kulinda usalama wa waandishi wa habari katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa Corona, wamiliki wa vyombo vya habari nchini wanapaswa kufanya yafuatayo;

- i) Kuhakikisha watumishi wanafuata maelekezo ya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huo yanayotolewa na wataalam wa afya.
- ii) Kuhakikisha watumishi wanapewa na kuvaa vifaa vya kujilinda dhidi ya maambukizi kama barakoa (mask) na glavu wanapokwenda kwenye maeneo hatarishi.
- iii) Kusimamia watumishi kuvaa vifaa vya kujikinga na maambukizi wanapokwenda kwenye maeneo ya mikusanyiko ikiwemo mikutano ya vyumba vya habari.
- iv) Kuhakikisha waandishi wanavaa vifaa vya kujikinga dhidi ya maambukizi wanapokwenda maeneo yenye wagonjwa au wahisiwa wa ugonjwa wa Corona.
- v) Kuhakikisha kuna maji yanayotiririka na sabuni kwa ajili ya watumishi kunawa na kuweka mikono yao safi wakati wote.
- vi) Kuhakikisha kuna vitakasa mikono (sanitizer) muda wote kwenye eneo la kazi kwa ajili ya kutumiwa na watumishi na wageni.

vii) Kutoa ruhusa na kuwashauri watumishi wenye kuonyesha dalili za kuwa na maambukizi kwenda vituo vya afya kupata huduma ikiwa ni pamoja na kufuatilia na kusimamia matibabu yao.

viii) Kutoa elimu ya mara kwa mara ya kuwakumbusha watumishi kujilinda na maambukizi ya ugonjwa wa Corona wanapokuwa ndani na nje ya maeneo ya kazi.

ix) Kuwatenga waandishi wa habari wanaokwenda kuripoti habari za magonjwa ya kuambukiza kwenye maeneo hatarishi na kuwakataza kuchanganyika na wenzao katika vyumba vya habari au watu wengine, kwa kipindi cha siku 14.

x) Kuepuka vipindi vinavyohusisha wageni katika vyumba vya habari. Kama ni lazima kuwa na washiriki kutoka nje kwenda chumba cha habari au studio, basi pawe na umbali wa zaidi ya mita moja (1) kati ya mshiriki mmoja na mwingine au kati ya mshiriki na mtangazaji. Waandishi wa habari au waendesha vipindi na waalikwa sharti wanawe mikono kabla na baada ya mahojiano na waepuke kugusa nyuso zao wakati wowote.

xi) Kuweka vitakasa mikono sehemu zote za kuingilia, msisitizo ukiwekwa zaidi kwenye milango ya kuingia chumba cha habari (Newsroom) na studio. Waandishi wa habari na waendesha vipindi pamoja na wageni waalikwa sharti watakase mikono kabla ya kuingia na kutoka. Wasaidizi wa vipindi sharti watakase mikono kabla na baada ya shughuli nzima ya kurusha kipindi na pale itakapoonekana ni lazima, wavae barakoa na glavu.



SURA YA 6



WAJIBU WA WAANDISHI WA HABARI NA WAPIGA PICHA KUJILINDA NA UGONJWA WA CORONA WAKIWA KAZINI

Waandishi wa habari wanapaswa kujilinda na maambukizi ya ugonjwa wa Corona kwa kufuata maelekezo yote ya wataalam wa afya pamoja na kufanya yafuatayo;

- i) Sikiliza na kufuata maelekezo ya wataalam wa afya unapokuwa kwenye maeneo hatarishi ya kazi.
- ii) Tumia vifaa vya kujikinga na maambukizi kama barakoa (mask) na glavu ukiwa kazini hasa kwenye maeneo hatarishi kama vile hospitali, kwenye maeneo ya misongamano, karantini n.k.
- iii) Tumia kinasa sauti kinachoshikiliwa na fimbo ndefu (boom mic) ukiwa umesimama kwa umbali wa zaidi ya mita moja.
- iv) Safisha vifaa vya kazi kama vile kamera, vinas sauti, taa, stendi za kamera na taa, vifaa vya kuchaji betri, headphone n.k ambavyo vinatumiwa kwa kushirikiana. Vifaa hivyo ni lazima vitakaswe kwa kutumia dawa maalum za kuu vimelea hatarishi kwa afya kabla na baada ya kutumika. Watumiaji wa vyombo hivi wavae glavu.



(v) Meza za waandishi, wapiga picha na wahariri, kompyuta, vichanganyio (mixers) na vifaa vingine vya kazi vitakaswe kwa kutumia dawa maalum za kuu vimelea hatarishi kabla na baada ya kutumika.

vi) Vifuniko au sponji za vinas sauti vinafaa pia kuoshwa vyema na kutakaswa baada ya kurejea kutoka kazi yoyote ya kuripoti. Tafuta ushauri/ mafunzo kuhusu jinsi ya kuvitoa vifuniko au sponji kwa njia salama kutoka kwa vinas sauti kuzuia kusambazwa zaidi kwa virusi.

vii) Tumia dawa maalum au kemikali za kuu vimelea hatarishi zenye Spirit.

viii) Takasa simu za mkononi, kompyuta mpakato, vihifadhia taarifa (hard drives), kamera, kompyuta, vitambulisho na kamba za kufungia vitambulisho.

ix) Hakikisha vifaa vyote vimetakaswa tena unapovirejesha ofisini na wanaovihifadhi wanajulishwa mapema na wanafundishwa namna ya kuvitakasa vifaa hivyo.

x) Unapotoka kufanya kazi kwenye maeneo hatarishi hakikisha unafanya usafi wa mwili kwa kuoga, kubadilisha nguo zilizovaliwa kazini na uzifue.

xi) Vua vito vyote na mapambo pamoja na saa kabla ya kwenda kazini kuripoti habari zinazohusu ugonjwa wa Corona kwenye maeneo hatarishi, ukikumbuka kwamba virusi vya Corona vinaweza kusalia vikiwa hai kwenye vitu vya aina nyingi.

xii) Upatapo dalili za maambukizi ya ugonjwa wa Corona hasa kikohozi, homa na shida ya kupumua usiende kazini, mtaarifu mwajiri wako na fika katika kituo cha kutolea huduma za afya au piga namba 199 au *199# kwa msaada.

xiii) Iwapo una historia ya kukutana au kugusana na mtu mwenye dalili za ugonjwa wa Corona au aliyethibitishwa kuwa na maambukizi ya ugonjwa wa Corona usiende kazini, toa taarifa haraka kwa mwajiri na ripoti kituo cha afya ili kupata ushauri na muongozo wa kitabibu. Hatua hii itasaidia kuzuia maambukizi kwa familia, wafanyakazi wenzako na jamii kwa ujumla kama utathibitika kuwa na maambukizi ya ugonjwa wa Corona.



SURA YA 7

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KWA WANAOKWENDA KURIPOTI HABARI ZA UGONJWA WA CORONA KWENYE MAENEO HATARISHI

Wakuu wa vyombo vya habari na wahariri wa habari wanapaswa kuzingatia yafuatayo wakati wa kugawa majukumu kwa watumishi wao kwenda kuripoti habari za mlipuko wa ugonjwa wa Corona kwenye maeneo hatarishi;

- i) Wazee, wajawazito na watu wenye matatizo mengine ya kiafya mfano magonjwa ya kisukari, moyo, kansa, figo na watu wanaoishi na VVU wasipangiwe kazi kwenye maeneo hatarishi kwa kuwa wakipata maambukizi wanaathirika zaidi, hivyo ni muhimu kuwakinga.
- ii) Viongozi wanashauriwa kutoa elimu ili kuepuka unyanyapaa wa waandishi wanaokwenda kuripoti matukio ya mlipuko wa ugonjwa wa Corona.
- iii) Wakuu wa vyombo vya habari wanashauriwa kutafuta wataalam wa saikolojia watakaoweza kutoa msaada wa kisaikolojia kwa watumishi katika kipindi cha majanga hususan kwa wale wanaoripoti habari za ugonjwa wa Corona.
- iv) Iwapo mwandishi/ mpiga picha anatembelea kituo cha afya chenye wagonjwa wenye maambukizi ya Corona, nyumbani kwa mtu anayeugua, eneo la karantini au mtaa wenye watu wengi anapaswa kuzingatia hatua za kudhibiti maambukizi kama kunawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka au kutakasa mikono kwa dawa maalum (sanitizer), kukaa umbali unaozidi mita moja (1) baina ya mtu na mtu bila kusahau kuvaa barakoa.
- v) Iwapo mwandishi au mpiga picha anafanya kazi katika eneo lililoathiriwa, kwa mfano kituo cha afya anaweza akahitaji viatu vya kuvaliwa kwa muda au atumie buti zisizoingiza maji za kuvaliwa juu ya viatu vya kawaida. Vyote ni lazima vipanguswe/ kusafishwa vyema baada ya kuondoka eneo hilo.
- vi) Mwandishi au mpiga picha atumie glavu za kuingia mikono iwapo anafanya kazi ndani ya eneo hatarishi kwa mfano kituo cha kuwatibu wagonjwa. Vifaa vingine vya kimatibabu vya kuingia mwili (PPE) kama vile vazi maalum la kuingia mwili dhidi ya maambukizi linalofunika mwili wote na barakoa inayofunika uso vinaweza kuvaliwa kwa ushauri wa wataalam wa afya iwapo mwandishi ameruhusiwa kutembelea maeneo hatarishi.
- vii) Baada ya kufanya kazi kwenye maeneo hatarishi, mwandishi au mpiga picha anapaswa kufuatilia hali yake ya afya mara kwa mara kubaini kama ana dalili za ugonjwa huu ili awahi kituo cha afya.
- viii) Iwapo mwandishi au mpiga picha amerejea kutoka eneo lililo na kiwango kikubwa cha maambukizi, kuna uwezekano mkubwa sana kwamba atalazimika kujitenga kwa kuzingatia maelekezo ya Serikali na wataalam wa afya.

ix) Ni muhimu kwa mwandishi au mpiga picha kutunza afya yake kipindi chote cha mlipuko wa ugonjwa wa Corona kwa kuzingatia:

- ♦ Lishe bora hasa inayojumuisha matunda na mboga za majani,
- ♦ Kufanya mazoezi,
- ♦ Kulala muda wa kutosha masaa nane (8),
- ♦ Kuepuka vilevi kama sigara, pombe na madawa ya kulevyana
- ♦ Kufanya mambo ya kutuliza akili ili kupunguza msongo wa mawazo.



SURA YA 8

8.0 MAMBO YA KUZINGATIA KATIKA KUHAKIKISHAA MAKUNDI MAALUM YA JAMII (WALEMAVU, WAZEE, WANAWAKE, WATOTO NA JAMII YA PEMBEZONI YANAELIMISHWA KUHUSU UGONJWA WA CORONA

Wanawake, wazee, vijana, watoto, watu wenye ulemavu na jamii za pembezo wanadhaniwa kuwa katika hatari zaidi wakati wa dharura na majanga kwa sababu ya ukosefu wa taarifa sahihi.

Utoaji taarifa juu ya hatari, kupanga mipango ya ushiriki wa jamii kwa jinsia, lugha, na tamaduni za mahali husika kunaboresha maarifa na uwezo wa jamii kuchukua hatua stahiki wakati wa majanga yakiwemo milipuko ya magonjwa.

Kuna masuala yakuzingatia kuhakikisha haki za binadamu na ushirikishwaji wa jamii yanazingatiwa katika upelekaji wa taarifa sahihi na kwa wakati kuhusu ugonjwa wa Corona kwa makundi tajwa hapo juu kama ifuatavyo;

8.1 Watoto

Watoto wasio na waangalizi na waliotengwa wanaweza kuwa katika hatari zaidi wakati wa majanga kwa kukosa taarifa na huduma zinazofaa kwa wakati. Kwa kawaida, watoto hawawezi kuelezea hofu yao au wasiwasi wao katika kipindi cha majanga. Vipindi vya muda mrefu vya kufungwa kwa shule vinaweza kuwasababisha mihemko na wasiwasi.

Kufadhaika kwa walezi kutokana na ugonjwa wa Corona kunaweza kusababisha kuongezeka kwa ukatili dhidi ya watoto nyumbani. Ikiwa walezi wameambukizwa inaongeza uhitaji wa usalama na msaada wa kisaikolojia zaidi kwa watoto.

Zingatia yafuatayo wakati wa kutoa taarifa ya kumuelimisha mtoto kuhusu ugonjwa wa Corona;

- Wasiliana/washirikishe watoto na vijana, pamoja na wale ambao wako katika mazingira hatarishi na waliotengwa, ili kuelewa wasiwasi wao, hofu na mahitaji yao.
- Tumia vyanzo sahihi kama invyoelekezwa na Serikali kutengeneza vipindi vinavyoel-keza sehemu sahahi ya kupata ushauri nasaha na huduma za msaada kwa wale walioathirika.
- Fikiria mahitaji tofauti ya watoto na vijana kulingana na jinsia, muktadha na jamii zilizotengwa.
- Andaa vipindi/makala za janga la corona vitakavyovutia watoto kusoma/kusikil-iza/kuangalia na kuelimika.
- Wape wazazi ustadi wa kushughulikia mahangaiko yao wenyewe na kusaidia kusimamia stadi hizo kwa watoto wao.

8.2 Watu wenye ulemavu:

Upataji wa habari za majanga kwa wakati mara nyingi huwa kizuizi kwa watu wenye ulemavu ambao wana mahitaji maalum ya mawasiliano.

Katika harakati za kuhakikisha kwamba hakuna anayeachwa nyuma kwenye kupambana na maambukizi ya ugonjwa wa corona yafuatayo yanapaswa kuzingatiwa:

- Kusanya maoni kutoka kwa watu wenye ulemavu.
- Andika au tangaza habari kwa kutumia lugha rahisi inayoeleweka.
- Toa habari katika muundo rafiki kama maandishi makubwa au video katika mitandao ya kijamii kwa wasiosikia.
- Zingatia ushauri wa wataalam wa huduma za jamii katika kutengeneza vipindi na makala za kuelimisha kundi hili la jamii.

8.3 Wanawake na wasichana:

Wanawake huunda sehemu kubwa ya wafanyakazi wa afya. Watunzaji wengi wa wagonjwa katika ngazi ya familia ni wanawake.

Wanawake ni washikiri wakubwa katika sekta isiyorasmi na huathirika zaidi kiuchumi katika kipindi cha majanga yakiwemo magonjwa ya mlipuko kama vile ugonjwa wa Corona. Wanawake wako katika hatari ya unyanyasaji wa kijinsia. Sababu za kiutamaduni zinaweza kuwatenga wanawake katika nafasi za maamuzi na kuzuia upatikanaji wao wa habari juu ya majanga yakiwemo magonjwa ya mlipuko.

Zingatia yafuatayo ili kusaidia kundi la Wanawake kupata taarifa sahihi zenye msaada kwao katika kukabiliana na changamoto za ugonjwa wa Corona;

- Hakikisha kwamba vipindi vya redio, televisheni au uandishi wa makala za magazetini unazingatia usawa wa kijinsia na kuimarisha nafasi ya wanawake katika harakati za kijamii na mapambano dhidi ya ugonjwa wa Corona.
- Andika habari au andaa vipindi vyenye ushauri mahususi utakaowasaidia wanawake wanaojali na kuuguza watoto, wazee na makundi mengine yaliyo hatari kupata ugonjwa wa Corona.
- Hakikisha unaandaa habari/vipindi kwa kuwashirikisha wanawake katika mahojiano ili kufahamu changamoto za kijamii na kiuchumi wanazokabiliana nazo na toa ushauri wa kuwasaidia kukabiliana na changamoto zao wakati wa mapambano dhidi ya ugonjwa wa Corona.

8.4 Wazee:

Kwa hali ya kawaida, Wazee wanahitaji matunzo ya ziada kwa kutegemea hali za familia au walezi. Kipindi hiki cha kukabiliana na ugonjwa wa Corona kinaweza kuwa kigumu zaidi kwa wazee iwapo hawatapata taarifa sahihi na kwa wakati juu ya tahadhari zinazotolewa ili kukabiliana na ugonjwa huu. Wazee pia wanaweza wasielewe habari kwa urahisi na kushindwa kufuata maagizo/maelekezo ya kujikinga.

Zingatia yafuatayo wakati unatengeneza taarifa kwa ajili ya kundi la Wazee;

- Tayarisha makala au kipindi chenye ujumbe unaoendana na hali halisi ya wazee ili waweze kujikinga na maradhi katika mazingira tofauti kama nyumbani, soko ni, hospitali, vituo vya basi au wakiwa kwenye shughuli nyingine.
- Shirikisha wazee kwa kushughulikia maoni na maswali yao maalum.
- Tengeneza ujumbe maalum unaoenga familia na watoa huduma ya afya kuelezea hatari ya ugonjwa wa Corona kwa wazee na jinsi ya kuwatunza.

8.5 Watu wenye magonjwa sugu:

Kwa ujumla watu wenye magonjwa sugu kama kisukari, figo, WU, pumu na ugonjwa wa moyo wako kwenye hatari kubwa ya kuathirika zaidi na ugonjwa wa Corona. Mara nyingi kundi hili hukosa habari sahihi na kwa wakati inayoelezea kwa nini wako kwenye hatari. Kundi hili lina uhitaji wa matibabu maalum na kutakiwa kufuata ushauri wa matibabu kila wakati.

Zingatia yafuatayo ili kuweza kufikisha ujumbe sahihi kwa kundi la watu wenye magonjwa sugu;

- Andaa Kipindi au habari ya mahitaji maalum inayoelemba kwa nini wenye magonjwa sugu wako kwenye hatari zaidi na namna ya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa Corona.
- Andaa kipindi au habari inayoelekeza familia namna ya kuwatunza iwapo watakata maambukizi ya ugonjwa wa Corona.
- Taarifa iwe inayo watia moyo na kuwahimiza kuchukua tahadhari na kufuata maelekezo ya wataalam wa afya kupata matibabu. Pia unaweza kuwapatia ushauri wa kisaikolojia kutoka kwa mwana saikolojia unayeweza kumhoji.

8.6 Jamii za pembezoni:

- Jamii ya watu wanaoishi maeneo ya pembezoni (Vulnerable communities) mwa nchi wako katika hatari zaidi ya kukosa taarifa za majanga.

Zingatia yafuatayo katika kutoa taarifa kwa kundi hili;

- Hakikisha unatumia lugha inayoeleweka na kundi la watu hao au tafsiri habari katika lugha za jamii husika wa maeneo ya pembezoni ili kurahisisha mawasiliano hususan katika kutoa tahadhari ya majanga.
- Toa fursa ya kupokea maswali yao na mawazo yao katika lugha yao. Hii ni pamoja na kuhakikisha ushiriki kamili wa wanawake wa maeneo hayo.

8.7 Kukabili unyanyapaa, ubaguzi na uzushi katika jamii:

Kuongezeka kwa uvumi hatarishi na unyanyapaa kunaweza kudhoofisha juhudi kubwa za mapambano dhidi ya ugonjwa wa Corona.

Zingatia yafuatayo ili kuzuia unyanyapaa kwa watu wanaougua au waliougua ugonjwa wa Corona;

- Saidia kueneza habari sahihi kufikia jamii zilizotengwa na/ au jamii zilizo katika mazingira hatarishi bila kuonyesha wazi kwamba zinalenga vikundi hivyo pekee.
- Epuka maneno: alama za kijiografia/ kabila (kwa mfano. Wuhan Virus), "mwathirika", "muambukiza" au "kaeneza kwa wengine".
- Rudia habari tu kulingana na taarifa/ takwimu ya kisayansi ya kuaminika na ushauri rasmi wa afya (tumia lugha rahisi na epuka maneno ya kiufundi) – tumia lugha nyepesi kukabili/kujibu habari na hisia za uongo pamoja na kuhimiza umuhimu wa kuzingatia njia sahihi ya kuzuia maambukizi.
- Tumia habari sahihi na za kuaminika zenye kuleta matumaini kwa makundi tofauti ya kijamii.

SURA YA 9

9.0. HITIMISHO:

Vyombo vya Habari ni mhimili muhimu katika kusaidia vita dhidi ya ugonjwa wa Corona (COVID-19). Afya ya watumishi wa vyombo vya habari ni muhimu kulindwa kwani kudorora kwa afya za watumishi hao kunaweza kudhoofisha juhudi za utoaji elimu kwa umma zinazoshirikisha vyombo hivyo. Maelezo haya yanalenga kuwakumbusha wamiliki na watumishi kujali afya na kujikinga na maambukizi. Aidha, maelekezo ya vitu vinavyopaswa kuzingatiwa wakati wa kuripoti taarifa zinazohusu ugonjwa wa Corona yamefafanuliwa. Maelekezo yaliyomo humu yanapaswa kuzingatiwa sambamba na miongozo mingine inayotolewa na Shirika la Afya Duniani (WHO) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.



Jikingo, Wakinge Wengine
CORONA INAZUILIKA

Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo
S.L.P 25,
Mji wa Serikali, Mtumba, Dodoma
Email: km@habari.go.tz